JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

MTWARA NOVEMBA, 2022

TAKUKURU MTWARA YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI YENYE THAMANI YA SH. BILIONI 10.

Katika kipindi cha Julai – Septemba 2022, TAKUKURU Mkoa wa Mtwara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, huku mkazo ukiwekwa katika UZUIAJI RUSHWA pamoja na elimu ya kuhamasisha wananchi washiriki kikamilifu hasa katika eneo la uwajibikaji na kuchukua hatua stahiki ili kuzuia rushwa, kwa kuwa jukumu la kuzuia rushwa ni la kila mmoja wetu kwa nafasi yake.

1. UZUIAJI RUSHWA:

Katika eneo la **UZUIAJI RUSHWA**, TAKUKURU Mkoa wa Mtwara **imefuatilia utekelezaji wa miradi ishirini na moja (21)** yenye thamani ya zaidi ya **shilingi bilioni 10** (10,002,188,576/=) katika sekta za Ujenzi, Elimu, Afya na Maji. Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Baadhi ya miradi iliyofuatiliwa ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:-

NA	WILAYA	MRADI	THAMANI
1	Mtwara	Mradi wa maji Mitambo - Msimbati Halmashauri ya Wilaya Mtwara.	654,796,775.90
2		Mradi wa barabara Kawawa Mkoani na Mkwawa Halmashauri ya manispaa ya Mtwara-Mikindani.	683,136,800/=

3	Masasi	Ujenzi wa barabara ya Mkapa kwa kiwango cha lami (km1) Halmashauri ya Mji Masasi	499,909,340/=
4		Ujenzi wa Kituo cha Afya Chikundi Halmashauri ya Wilaya Masasi.	250,000,000/=
5	Newala	Ujenzi wa barabara kiduni-Makonde-Mkunya	874,641,000/=
6		Mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji halmashauri ya mji Newala.	2,326,983,509.10
7	Tandahimba	Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa Afya hosipitali ya wilaya Tandahimba.	90,000,000/=
8	Nanyumbu	Ujenzi wa barabara ya Bomani na Mangaka-Nachingwea	994,833,784.70
9		Ujenzi wa Mradi wa maji Mitumbati-Chilunda	1,356,000,537.80

Miradi 3 (sawa na asilimia 14), ilikuwa na mapungufu madogo kama kuchelewa kukamilika kwa mujibu wa mkataba, jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama, matumizi ya vifaa visivyokidhi ubora pamoja, manunuzi kwa gharama zaidi ya bei ya soko na kutofanyika kwa baadhi ya kazi zilizoelekezwa kwenye BOQ.

Mapungufu katika miradi mitatu yalirekebishwa kwa kutoa elimu kwa wajumbe wa kamati zinazohusika katika ujenzi, kuhusu umuhimu wa kushirikiana na kusimamia mradi kwa pamoja na kuhakikisha malipo kwa kazi au huduma iliyokamilika yanafanywa kwa wakati. Na pia mamlaka zimetakiwa kutofanya malipo kwa kazi ambazo hazijafanyika.

1.1 UCHAMBUZI WA MIFUMO:

Pale ambapo eneo la utendaji au utoaji huduma linaonekana au kulalamikiwa kuwa na viashiria vya rushwa, TAKUKURU hufanya **uchambuzi wa mfumo** ili kubaini iwapo kuna mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuiziba. Hivyo katika kipindi husika:-

- Tumefanya **chambuzi nne** za mifumo katika sekta ya kilimo, ushirika, ujenzi na Afya.
- Tumebaini kwamba kwenye uchambuzi wa mfumo wa manunuzi kwa kutumia njia ya 'force account' katika miradi ya afya, kuna

ufahamu mdogo kwa kamati za hosipitali kuhusu mfumo huu katika manunuzi.

- Kwenye uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, imebainika kuwa kuna utoaji wa mikopo, uingiaji wa mikataba na uongozi usiyofuta sheria, kanuni na taratibu za vyama vya ushirika.
- Kwenye uchambuzi wa mfumo wa utoaji dawa na vifaa tiba katika hosipitali, kuna baadhi ya dawa na vifaa tiba hutolewa stoo bila 'issue voucher' kusainiwa na afisa anayeomba na kupokea dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kwenda kutumia kwa wagonjwa.
- Vilevile baadhi ya dawa zinatolewa stoo lakini hazionekeni katika rejista ya kutolea dawa kwa wagonjwa (Dispensing register).

1.2 WARSHA ZA WADAU:

Warsha 3 za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mifumo kwa kushirikisha wadau zilifanyika katika sekta ya ujenzi na afya ambapo maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa yalifikiwa na muda wa utekelezaji kuwekwa.

Vilevile, **taarifa mbili** za utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa siku za nyuma katika sekta za elimu na afya zilipokelewa.

Kupitia taarifa hii, tunawakumbusha wote wenye wajibu wa kufanyia kazi maazimio ya kuziba mianya ya rushwa bainishwa, kutekeleza wajibu wao kwa wakati.

2. UELIMISHAJI UMMA:

Kazi za Uelimishaji Umma zilizofanyika ni zifuatazo:-

NA	KAZI	UFAFANUZI
1	Kutembelea na kuimarisha klabu za wapinga Rushwa katika shule za msingi na Sekondari na vyuo.	klabu za wapinga Rushwa 39 zilizopo katika shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo ziliimarishwa kwa kupewa elimu ya kukuza uzalendo na uadilifu.
2	Kufanya maonesho mawili.	Katika maonesho haya Elimu ilitolewa ambapo Wananchi walikumbushwa juu ya jukumu la kuzuia Rushwa na namna wanavyoweza kushirikiana na TAKUKURU katika kuzuia Rushwa na

		wananchi pia walipata fursa ya kutoa maoni yao juu ya namna ya kuboresha ushirikiano ili kudhibiti vitendo vya rushwa.
3	Mikutano ya hadhara vijijini ili kuwafikia wananchi wengi walioko pembezoni.	Ilifanyika mikutano ya hadhara 11 ambapo wananchi walihimizwa kushiriki na kusimamia miradi ya maendeleo ili kuzuia rushwa na zaidi kuhudhuria mikutano ya vijiji ili kutoa michango yao na kuhoji mapato na matumizi ya kijiji pale ambapo wanaona kuna shida.
4	Semina watumishi wa umma makazini na kutoa elimu juu ya rushwa mahala pa kazi.	Semina 44 zilitolewa kwa lengo la kuwakumbusha watumishi kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo na kujiepusha na vitendo vya Rushwa.
5	Utoaji wa habari na makala.	Makala 4 na taarifa kwa umma 2 zilitolewa ili kufahamisha umma juu ya mambo mbalimbali yanayofanyika katika uzuiaji rushwa pamoja na kuhabarisha umma juu ya utendaji wa TAKUKURU (M) Mtwara.

Vilevile elimu ya rushwa ilitolewa kwa wateja wanaotembelea ofisi zetu na kutaka ushauri na machapisho mbalimbali kwa ajili ya rejea.

2.1 TAKUKURU INAYOTEMBEA

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara kwa ushirikiano na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, ilifanikiwa kutembelea Baraza la Kata ya Mbawala baada ya kupokea malalamiko mengi ambayo kimsingi yalitokana na baadhi ya wajumbe wa baraza hilo kutoelewa mabadiliko ya sheria ambapo kwa sasa mabaraza hayo yanafanya kazi ya usuluhishi na sio kutoa hukumu. Mwanasheria wa Halmashauri aliwapa elimu hii na kuwataka wazingatie ikiwemo kurekebisha pale walipokosea. Aidha wajumbe wa baraza walielimishwa kuhusu makosa ya rushwa hasa kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA:

Pamoja na kuhamasisha sana suala la **KUZUIA RUSHWA,** bado wapo ambao hufanya TAKUKURU ilazimike kufanya kazi za mapambano dhidi ya Rushwa.

Katika kipindi husika, tumepokea **malalamiko 64,** ambapo **taarifa za rushwa zilikuwa 41** na **zisizo za rushwa ni 25.**

- Taarifa 41 zinazohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo: Ushirika (10); Utawala (08); Elimu (7); Mahakama (6); Afya (3); Maji (2), Siasa (1) na Sekta binafsi (4).

- Taarifa 41 zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria kwa kuanzisha uchunguzi.

- Kupitia uchunguzi huo, Majalada 3 yamekamilika na **mashauri 7** mapya yamefunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani kufikia **18.**

- Idadi ya mashauri yaliyoamuliwa katika kipindi hiki ni **matatu** ambapo Jamhuri ilishinda katika mashauri **mawili.**

- Kati ya taarifa **25** zisizohusu rushwa, wahusika walishauriwa mahali sahihi pa kuziwasilisha na wengine walieleweshwa na kuridhika hivyo taarifa hizo zikafungwa.

Katika hatua nyingine: Katika hali inayoonesha wazi kuwa Rushwa hailipi ni pale ambapo washtakiwa katika kesi Na. ECC 01/2022 iliyotolewa hukumu Tarehe 01/08/2022 na washtakiwa kukutwa na hatia baada ya kufanya maridhiano ya kukiri kosa (Plea bargaining) na hivyo kutakiwa kulipa kiasi cha shilingi milioni kumi kwa ubadhirifu wa shilingi milioni tatu laki tisa na elfu kumi na tano. Aidha washtakiwa walihukumiwa pia kwenda jela miezi miwili.

Aidha katika kesi nyingine Na. ECC 02/2022 mshtakiwa pamoja na kusomewa hukumu ya kulipa faini ya shilingi 200,000/= au kwenda jela mwaka mmoja, alitakiwa pia kurejesha kiasi cha shilingi 6,042,340.47 alizofanyia ubadhirifu na uchepushaji. Huu ni ujumbe tosha kwamba

Rushwa hailipi na hivyo ni bora kuepuka vitendo vya rushwa kwani gharama yake ni kubwa zaidi.

4. MIKAKATI YA OKTOBA– DESEMBA 2022:

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, inatarajia katika robo ya Oktoba-Desemba, 2022, kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kukagua miradi ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo vipindi vya redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na matumizi ya fedha za umma na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma. Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

Pia tumejipanga kupitia mpango wetu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA, kupita kwenye mabaraza ya kata na vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS), kwa kushirikiana na Wakurugenzi, Wanasheria na Maafisa Ushirika wa halmashauri husika, ili kutoa elimu ya rushwa na mabadiliko ya sheria kwa lengo la kuzuia rushwa na kuboresha usuluhishi wa migogoro ya ardhi katika kata zetu na kuainisha na kuziba mianya ya rushwa katika vyama vya ushirika.

5. HITIMISHO:

Mwisho, tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kutuunga mkono katika vita hii yetu sote. Tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee waachane na fikra hizo batili na wajiunge nasi ili kuongeza nguvu katika jeshi la wazalendo, waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa. Umoja ni nguvu. **RUSHWA HAILIPI**.

Imetolewa

ENOCK P. NGAILO
MKUU WA TAKUKURU (M) MTWARA
0738150156